

Vijana wapo katika kipindi cha mpito cha kubadilika kutoka utotoni kwenda kwa utu uzima, ni ukweli usiopingika kuwa maisha haya ya ujana huambatana na changamoto nyingi sana ambazo kwa haraka utagundua kuwa vijana wenyewe huwa ni kana kwamba hawazitambui hizo changamoto bali wanaoumia ni wale wasimamizi wao wa karibu, wakiwemo wazazi, walezi, walimu na viongozi wa dini.

Mfano wa changamoto ni kuanza kujihusisha na mambo yasiyofaa kama vile ngono za utotoni na tena kabla ya kuingia kwenye ndoa, ambapo mwisho wake ni kupata ujauzito na wengine hupata magonjwa ya zinaa, ikiwemo UKIMWI, Zaidi ya hapo wengine hupotoka kimaadili kwa kuijingiza kwenye matumizi ya madawa ya kulevyta na kuiga mitindo ya maisha isiyofaa katika jamii. Wazazi wengi majumbani wanalia kwa kutokuwa na uhusiano mwema na watoto wao hasa ambao wanaingia katika umri wa ujana, sababu watoto hawawasikilizi, na tena wengine huthubutu hata kuondoka nyumbani na kujianzishia maisha yao wenyewe, japokuwa wengi wao unakuta bado hajawawa na uwezo wa kujitegemea kiuchumi.

Ni kwa nini inakuwa hivyo? Ni kwa sababu vijana kwa wakati huo hujiona ni tayari wamefanikiwa na wanatamani kuwa na uhuru wao binafsi, hawapendi kuingiliwa. Vijana hupenda kuwa na ratiba yao wenyewe mfano wanapokuwa nyumbani hawapendi kupangiwa aina ya mavazi ya kuva, hata chakula wanapenda kula kile ambacho wanapendelea. Kama ni binti anatamani kuwa mwanamke kwenye nyumba yake mwenyewe, lakini kama ni kijana atatamani kuwa mwanaume katika nyumba yake mwenyewe.

Malalamiko ya wazazi wengi kwa vijana wao, ni juu ya ukaidi wa vijana hawa kupangiwa majukumu ya nyumbani na kugoma kuyafanya, au kufanya kwa unyonge, lakini si majukumu ya kupangiwa tu, bali hata yale yanayoonekana kuwa kwa faida yao wenyewe. Mfano wapo ambao wamekataa kuendelea na masomo japokuwa unakuta mzazi ana uwezo wa kulipa ada zote, ama si kulipa ada wengine unakuta keshalipa kabisa, lakini kijana anaamua kuachana na masomo.

Je ni nini kinawatokea vijana wetu? Ni maswali magumu na yasiyokuwa na majibu ambayo wazazi wengi hujiuliza na bado hubaki bila kuwa na majibu ya kuwatoshaleza juu ya vijana wao, ndipo huendelea kutafuta suluhu la kuhakisha kuwa vijana wanarejea katika mstari ulionyooka. Siku moja nilikutana na mzazi mmoja ambaye sitamtaja akaniomba nifanye maombi maalum kwa kijana wake ambaye alikuwa ameamua kuacha masomo ya sekondari na ameingia mtaani kufanya biashara, ambayo ilionekana ni kana kwamba hailipi, na mzazi hakika aliona mwanaae amepotea.

Kwa kusoma kitabu hiki kinatoa namna ambavyo kijana anapitia hatua mbalimbali za makuzi ya kimwili, kiakili, kijamii, kielimu, na kimaadili, utaona pia jinsi ambavyo kijana anaweza kufanya uchaguzi wa kazi ambayo anaipendelea, hata kama inaonekana kuwa ni duni au kazi isiyokuwa na mapato ya kutosha, ni bora kufanya aina hiyo ya kazi kuliko kufanya kazi yenye pesa za kutosha lakini haileti furaha kwa muhusika. Karibu sana ubarikiwe na kitabu cha "Saikojia ya Vijana"ni mjoli wako shambani mwa Bwana:



Edit with WPS Office

Chacha Isaac Mtiti.

E-mail- mtitijunior@gmail.com

Simu: 0754761229/0629728708.



Edit with WPS Office